



**MREMBO WA DUNIA, MREMBO WA TANZANIA PAMOJA NA
MHESHIMIWA DR. HERSON MWAKYEMBE, MPO ARUSHA KWA
UZINDUZI WA HEDHI RAFIKI, YENYE AFYA KWA WASICHANA**

*Ujio wa shirika la mrembo wa dunia unawakilisha uzinduzi kwa
Tanzania*

VYOMBO VYA HABARI

Basilla Mwanukuzi

255-713-430-331

TheLookCompany2018@gmail.com

Oktoba 28, 2019. Arusha, Tanzania Siku ya Leo, UhuruPads – Pedi za hedhi pekee zinazoweza kuoza kwa 100% zikitupwa ambazo zinatengenezwa nchini – walifanya uzinduzi katika shule ya sekondari ya Moshono mjini Arusha. Zaidi ya wasichana 400 walipokea pedi hizi za hedhi ambazo ni rafiki kwa mazingira, nguo za ndani pamoja na taarifa zingine za usafi.

Baadhi ya wageni waalikwa walikuwa ni:



Sylvia Sebastian
*Reigning Miss
Tanzania*



Vanessa Ponce
kutoka Mexico
ambaye ni Miss World



Waziri wa Habari,
Utamaduni, Sanaa &
Michezo Dr. Harrison
George Mwakyembe



Julia Morley Mwenyekiti
wa Shirika la Miss World

Teknolojia na mfumo uliopo nyuma ya UhuruPads vilitengenezwa na Aakar Innovations kutoka Mumbai, India. Aakar ni raisi na mwanzilishi, Jaydeep Mandal alikuwepo. Mnamo mwaka 2017, mfumo wa Aakar ulizinduliwa nchini Tanzania na mjasiliamali wa kijamii kutoka Marekani, **Laura Chauvin**, akifanya kazi na mwanamichezo aliyeshiriki michezo 8 ya Wachezaji wote Nyota wa NBA, **Dwight Howard** (wa Los Angeles Lakers) alitoa udhamini wa fedha ili kuunga mkono juhudi za kikundi cha wanawake wa hapa nchini. Kwa hivi sasa timu ya wanawake 12 mjini Arusha inaunda timu ya Uhuru Kit Ltd., wakitengeneza pedi hizi rafiki kwa mazingira za UhuruPads zaidi ya 2000 kwa siku kwa ajili ya kutoa msaada kwa wasichana ili waweze kuhudhuria masomo yao shuleni hata katika siku zao za hedhi wakiwa na ujasiri. Vitu vyote vinavyounda bidhaa hii vinauwezo wa kuoza vikitupwa, hivyo kusaidia wasichana bila kuongeza changamoto zingine za kimazingira.

Shirika la Miss World ni watetezi wakubwa katika masuala ya usafi wa hedhi ili kulinda heshima ya wasichana na kuhakikisha wanapata elimu ikiwa ni sehemu ya kampeni yao ya “Beauty with a Purpose”. Shirika la Miss World limeshawishi pia wawakilishi wengine wa shirika hilo – akiwemo Miss World, **Vanessa Ponce kutoka Mexico na Miss Tanzania, Sylvia Sebastian** – wawe



UhuruPads is an initiative of the non-profit Foot Forward Fund, a US 501c3. Operating in East Africa as Uhuru Kit, Ltd., UhuruPads has secured all governmental licenses for production, sales, and humanitarian distribution.
www.UhuruPads.org

MEMBER





mstari wa mbele kusimamia bidhaa hii ya kibunifu ya usafi wa hedhi pamoja na elimu ndani ya nchi zao.

Mwenyekiti wa Miss World – **Mrs. Julia Morley** – amefurahi sana kwa shirika lake kutembelea kwa mara ya kwanza nchini, pamoja na mrembo anayeshikilia taji la Miss World na Miss Tanzania. Miss World **Vanessa Ponce**, amesema “Duniani, takribani tani 113,000 za taulo za wanawake zinatupwa kila mwaka, na kuchafua mazingira yetu. Lakini pia ni muhimu sana kwa wasichana kuelewa umuhimu wa afya bora katika masuala ya hedhi; Sote tuna jukumu muhimu la kijamii kunyoosha mkono na kusaidiana.” Miss Tanzania, Sylvia Sebastian, alisema: “Bidhaa hii imekuja muda muafaka na kwa dhumuni sahihi. Kusaidia wasichana wetu wabaki shuleni na kufuata ndoto zao ni muhimu sana. Kuweza kufanya hayo na kwa wakati huo huo kuhifadhi mazingira na pia kutoa ajira kwa wanawake ni jambo la nyongeza.”

Zaidi ya wasichana wa Kitanzania 4000 tayari wanapokea UhuruPads na elimu ya usafi na afya. Viongozi wa shule ya Moshono wameongea kwa nguvu juu ya changamoto hiyo ya kipekee ambayo inawakabili wasichana wao wakati wa mzunguko wao wa hedhi. Wasichana wanaweza kukosa mpaka siku nne za masomo yao shuleni katika kipindi cha hedhi.

Dr. Harrison George Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa & Michezo, na moja wa wabunge Bungeni pia alitoa kauli za kuunga mkono fursa hii kwa wanawake na wasichana. Video inayoonyesha mchakato wa utengenezaji wa pedi hizo ilionyeshwa na mipango ya kiwanda kipya na cha kisasa cha UhuruPads – kitakachofadhiliwa na Shirika lisilo la kiserikali pamoja na kujengwa katika eneo la **WorldServe International** – ilionyeshwa.

Usafiri wa wajumbe wote wa Miss World uliwezesha na Roy Safaris, Ltd., huku makazi katika hoteli na vyakula vikitolewa na African Tulip Hotel ya Arusha.

Moshono Secondary School, Arusha
Latitude 3.3898087⁰ Longitude 36.730226⁰
Or URM 37M 270037 9625074

UhuruPads is an initiative of the non-profit Foot Forward Fund, a US 501c3. Operating in East Africa as Uhuru Kit, Ltd., UhuruPads has secured all governmental licenses for production, sales, and humanitarian distribution.
www.UhuruPads.org

MEMBER



AFRICAN COALITION
FOR MENSTRUAL
HEALTH MANAGEMENT